



## Maswali Na majibu kuhusu uenezaji wa virusi kutoka kwa mama hadi mwanaye (MTCT)

Q. MTCT ni nini?

Hii ni uenezaji wa virusi vya ukimwi kutoka kwa mamas hadi mwanaye ambaye hajazaliwa . kama mama ni mja mzito kuna asilimia thelathini ya kwamba atamuambukiza mtoto virusi hivi. Mtoto anaweza pata virusi hivi wakati mama an amimba,wakati wa kuzaa na wakati mtoto ana nyonyeshwa , asilimia sitini na tano ya watoto huambukizwa virusi wakati wa kuzaliwa.

Q. Hii huzuiwa aje?

Kuna njia nne ya kuzuia ,kwanza ni kuwaeleza na wasichana na wamama njia za kujinga , pia kutumia kinga wakati wa kufanya mapenzi ili kuzuia mimba. Tatu ni wamama waja wazito wanapaswa kupimwa virusi hivi ili kujua hali. Na mwisho mama yeyote mja mzito mwenye virusi vya ukimwi ana paswa kutumia njia za kujikinga , ingawa njia hizi si kamili ,zinasaidia uambukizaji wa virusi.

Q. Je kuna utafiti wowote?

Ndio. Mama akitumia dawa ya AZT kabla ya kuzaa,hii huteremsha uambukizaji na aslimia sitini. Utafiti huko Ivory Coast, Uganda, na Burkina Faso umeonyesha uambukizaji umeshuka na asilimia thelathini na saba hadi arubaini na saba.

Q. Nini itafanyika nikiwa na mimba na niko na virusi vya ukimwi?

Kuna madawa ambazo mama hupatiwa wakati ana mimba na pia wakati wa kuzaa. Pia ni vizuri kumnyonyesha mtoto hadi miezi sita halafu kuwacha kabisa na kuanza kumpatia vyakula vingine ili kuteremsha hatari ya kumuambukizia virusi. Matibabu kama nevirapine pia inaonyesha kuteremsha uambukizaji na asilimia hamsini na hii ndio njia rahisi inayotumia na mataifa maskkini.

Q. Je hii ni njia ya muhimu ya kuteremsha uambukiza wa virusi vya ukimwi?

Ndio ,Na njia hii ina nia kwani mama anaweza zuia kumuambukizia mwanaye virusi , mwaka wa 2005 UNAIDS ili andika yakwamba watoto 700,000 chini ya miaka 15 wanaishi na virusi vya ukimwi ,wengi wa watoto hawa waliambukizwa virusi hivi na mama zao.Na wengi wa watoto hawa wanaishi nchi zinazoendelea.